




**RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA  
HESABU ZA SERIKALI**

**UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA  
ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI 2017**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora, S.L.P. 9080, Dar es Salaam. Simu ya Upopo: 'Ukaguzi' Simu: 255(022)2115157/8, Tarakishi: 255(022)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

Kwa Majibu Tafadhalii Nukuu

Kumb.Na. FA 27/249/01/2016/2017

31 Machi 2018

Mh. Dkt. John Pombe Magufuli,  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
Ikulu,  
S.L.P. 9120,  
1 Barabara ya Barack Obama,  
**11400 DAR ES SALAAM.**

**Yah: Kuwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2017**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) na Kifungu cha 34 (1)(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 (kama ilivyorekebishwa), ninawasilisha kwako ripoti ya saba inayohusu miradi ya maendeleo kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2017.

Nawasilisha.

**Prof. Mussa J. Assad**

**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,  
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,  
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

**(Ilianzzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)**

Madaraka na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali vimeelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kama ilivyorekebishwa) na kufafanuliwa zaidi katika Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 (kama ilivyorekebishwa) pamoja na Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009.

**Dira**

Kuwa Taasisi ya Hali ya Juu Katika Ukaguzi wa Sekta ya Umma.

**Dhamira**

Kutoa Huduma ya Ukaguzi wa Hesabu Yenye Tija ili Kuimarisha Uwajibikaji na Thamani ya Fedha Katika Kukusanya na Kutumia Rasilimali za Umma.

**Katika kutoa huduma zenyе ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:**

- **Uadilifu:** Sisi ni asasi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyo na upendeleo.
- **Ubora:** Sisi ni weledi tunaotoa huduma zenyе ubora kwa kuzingatia viwango kubalifu vya ukaguzi.
- **Uaminifu:** Tunazingatia na kudumisha kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala wa sheria.
- **Kuwalenga watu:** Tunamakinikia zaidi matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.
- **Uvumbuzi:** Sisi ni asasi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya asasi.
- **Matumizi bora ya rasilimali:** Sisi ni asasi inayothamini na kutumia rasilimali za umma ilizokabidhiwa kwa umakini mkubwa.

**Tunatimiza haya kwa kufanya yafuatayo:-**

- Kuchangia katika matumizi bora ya fedha za umma kwa kuhakikisha kwamba wakaguliwa wetu wanawajibika kutunza rasilimali walizokabidhiwa;
- Kusaidia kuimarisha ubora wa utoaji huduma kwa kuchangia ubunifu kwa matumizi bora ya rasilimali za umma;

- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wadau wetu kuhusu mapungufu katika uendeshaji wa shughuli zao;
- Kuwahusisha wadau wetu katika mfumo wa ukaguzi; na
- Kuwapa wakaguzi nyenzo za kufanya kazi ambazo zitaimarisha uhuru wa ofisi ya ukaguzi.

© Kwa mujibu wa Kifungu cha 39 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 (ilivyorekebishwa), Ripoti hii imekusudiwa kwa matumizi ya Mamlaka za Serikali. Hata hivyo, mara baada ya kupokelewa na Spika na kuwasilishwa Bungeni, ripoti hii huwa ni kumbukumbu ya umma na usambazaji wake hauwezi kuzuiwa.

## **Yaliyomo**

Dira.....	i
Dhamira .....	i
Orodha ya Majedwali .....	v
Vifupisho.....	vi
Dibaji .....	viii
Shukrani .....	x
i.Utangulizi .....	xii
ii. Hoja Muhimu Zilizojitokeza Wakati Wa Ukagazi .....	xii
iii. Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukagazi Yatokanayo na Ripoti za Kaguzi za Miaka Iliyopita .....	xv
iv. Mwelekeo wa Hati za Ukagazi Zilizotolewa.....	xvi
 SURA YA KWANZA.....	1
USULI NA TAARIFA ZA UJUMLA .....	1
1.0    Utangulizi .....	1
1.1    Mamlaka na Umuhimu wa Ukagazi .....	1
1.2    Wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali .....	2
1.3    Muundo wa Kazi za Ukagazi katika Ofisi ya Taifa ya Ukagazi .....	2
1.4    Mawanda na Viwango vya Ukagazi Vinavyotumika .....	3
1.5    Wajibu wa Maafisa Masuuli .....	4
 SURA YA PILI .....	5
HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA RIPOTI ZA KAGUZI ZA MIAKA YA NYUMA .	5
2.0    Utangulizi .....	5
2.1    Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi Zilizopita .....	5
 SURA YA TATU .....	8
AINA NA MWENENDO WA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA .....	8
3.0    Utangulizi .....	8
3.1    Aina za Hati za Ukagazi .....	9
3.2    Mwelekeo wa Hati za Ukagazi.....	11
3.3    Vigezo Vilivyo Sababisha Kutoa Hati Za Mashaka Na Hati Zisidhoridhisha.....	12
 SURA YA NNE .....	13
UTENDAJI WA KIFEDHA WA MIRADI .....	13
4.0    Utangulizi .....	13
4.1    Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) .....	13
4.2    Fedha za Mfuko wa Afya (HBF).....	15
4.3    Mfuko wa Barabara .....	17
4.4    Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya Tatoo - Mpango Uhaulishaji wa Fedha kwa Kaya Maskini .....	19
4.5    Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP).....	20
4.6    Miradi Mingine .....	23

SURA YA TANO .....	24
MUHTASARI WA MATOKEO YA UKAGUZI.....	24
5.0    Utangulizi .....	24
5.1    Masuala ya Usimamizi wa Fedha na Bajeti .....	24
5.2    Masuala Yanayohusu Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba .....	27
5.3    Utekelezaji wa Miradi .....	29
 SURA YA SITA .....	30
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....	30
6.0    Utangulizi .....	30
6.1    Hitimisho la Jumla.....	30
6.2    Mapendekezo ya Jumla .....	32
 VIAMBATISHO .....	35

## Orodha ya Majedwali


Jedwali Na. 1: Utekelezaji wa Mapendekezo Katika Ripoti za Kaguzi za Miaka ya Nyuma .....	6
Jedwali Na 2: Muhtasari wa Hati za Ukaguzi Zilizotolewa .....	9
Jedwali Na. 3: Mwelekeo wa hoja za ukaguzi .....	12
Jedwali Na. 4: Jumla ya Fedha za Mpango wa Maendeleo Sekta ya Kilimo Zilizopokelewa na Kuhamishwa .....	14
Jedwali Na. 5: Jumla ya Fedha Zilizokusanywa Kutumwa Mfuko wa Uchangiaji wa Afya .....	16
Jedwali Na. 6: Fedha zilizotumwa kwa Watekelezaji wa Miradi.....	17
Jedwali Na. 7: Mwenendo wa Makusanyo ya mapato kwa Miaka.....	18
Jedwali Na. 8: Ufadhilli wa Mfuko Mradi wa Maendeleo ya Jamii .....	20
Jedwali Na. 9: Vyanzo vya Fedha Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji .....	21
Jedwali Na. 10: Ufadhilli.....	22

## Vifupisho

AfDB	Benki ya Afrika ya Maendeleo Afrika
AFROSAI-E	Umoja wa Taasisi za ukaguzi Afrika Zinazozungumza Kiingereza
ASDP	Programu ya Maendeleo katika Sekta ya Kilimo
CCHP	Mpango Kabambe wa Afya
DADPs	Mipango ya Maendeleo ya Kilimo katika Wilaya
DFID	Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza
DK	Dola za Kimarekani
GIZ	Shirika la Kijamii la Kijerumani la Ushirikiano wa Kimataifa
Global Fund	Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria, UKIMWI na Kifua Kikuu
HBF	Mfuko wa Uchangiaji wa Afya
IDA	Shirika la Maendeleo la Kimataifa
IFAC	Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu na Wakaguzi
IFAD	Mfuko wa Kimataifa kwa Maedeleo ya Kilimo
INTOSAI	Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi
ISSAIs	Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi vya Ofisi za Ukaguzi wa Umma
JICA	Shirika la Maendeleo la Nchi ya Japani
JMT	Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
LAAC	Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa
LGFM	Randama ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa
NAOT	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi
NWIF	Mfuko wa Uwekezaji wa Maji Kitaifa
OPEC	Umoja wa Nchi Zinazozalisha Mafuta
PAA	Eneo la Mamlaka la Mradi
PAC	Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali
RSSP	Programu ya Msaada katika Sekta ya Barabara
SDR	Haki ya kutoa fedha
Sh.	Shilingi za Kitanzania
SNAO	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Sweden

TAMISEMI	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
TANROADS	Wakala wa Barabara Tanzania
TASAF	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii
TEMESA	Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania
TPRS	Mpango wa kupunguza Umaskini Tanazania
TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania
TSSP	Programu ya Msaada wa Sekta ya Usafiri
UN	Umoja wa Mataifa
UNDP	Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa
UNICEF	Sherika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto
USAID	Shirika la Misaada la Watu wa Marekani
VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani
WB	Benki ya Dunia
WSDP	Programu ya Maendeleo katika Sekta ya Maji

## Dibaji



Taarifa hii ni majumuisho ya matokeo ya kaguzi za miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017. Hii ni taarifa ya saba ya miradi ya maendeleo ambayo inajumuisha miradi mikubwa minne inayofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) na Wahisani wa Maendeleo kupitia mifuko ya pamoja na Mfuko wa Barabara ambao huchangiwa na chanzo cha mapato ya ndani yatokanayo na kodi ya mafuta. Miradi minne ya maendeleo ambayo huchangiwa kwa pamoja ni Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP), Mfuko wa Uchangiaji wa Afya (HBF), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP). Aidha, tumekaza miradi mingine inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Africa, Wakala wa Umoja wa Mataifa (UN), na makubaliano ya kifedha baina ya nchi mbalimbali.

Ripoti hii ya ukaguzi itawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) na Kifungu 34(1) & (2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008. Inajumuisha taarifa muhimu zilizo katika ripoti za ukaguzi walizopewa menejimenti za watekeleza miradi.

Ni matarajio yangu kuwa ripoti hii itawasaidia wadau wa miradi ya maendeleo kuweza kutathimini kama fedha zimetumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Pia itasaidia kutathmini mchango katika maendeleo ya jamii kiuchumi. Aidha, itasaidia kutathmini kama thamani ya fedha imepatikana.

Kwa mujibu wa Ibara ya 143(2)(c)(4) ya Katiba ya JMT ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa), Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa, angalau mara moja kila mwaka, kufanya ukaguzi na kutoa taarifa ya ukaguzi wa hesabu hizo kwa Rais wa JMT ambaye ataiwasilisha bungeni.

Aidha, uhuru wa ofisi yangu umeimarika katika kutimiza jukumu lake la kikatiba kutokana na kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 na Kanuni zake za mwaka 2009. Hata hivyo, jitihada zinahitajika ili kuboresha rasilimali za kufanya kazi ili kunisaidia kufanya vyema katika kutekeleza majukumu na wajibu wangu wa kikatiba.

Natarajia kuwa Serikali, Bunge, washirika wa maendeleo na umma kwa ujumla watachukulia taarifa hii kuwa ni muhimu katika kuelewa jinsi maafisa masuuli wanavyosimamia miradi ya maendeleo na namna mafanikio katika miradi ya maendeleo yanavyosaidia katika kutatua matatizo yanayowakabili Watanzania. Hivyo, ili kuboresha ripoti hii siku zijazo nitashukuru kupata maoni kutoka kwa jamii na watumiaji wengine wa taarifa hii kwa muda muafaka.



**Prof. Mussa Juma Assad**  
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

---

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,  
Dar es Salaam,

**Machi, 2018**

## Shukrani

Natoa shukrani za dhati kwa wadau wetu walioituwezesha katika kutuwezesha kutimiza majukumu yetu ya kikatiba. Nao ni pamoja na Bunge na kamati zake, hususani Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na Kamati ya Bunge ya Bajeti, Mlipaji Mkuu wa Serikali, Maafisa Masuuli wote wa wizara, mashirika ya umma na tawala za mikoa ambao wanasi mamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na walipa kodi.

Napenda kutoa shukrani zangu kwa watumishi wa ofisi yangu kwa kujitolea na kujituma katika kutimiza majukumu yetu ya kikatiba. Ni matumaini yangu kuwa wataendelea kutoa huduma ya kutosha na yenye ufanisi katika ukaguzi ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji na matumizi ya rasilimali za umma.

Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa wafadhili, hasa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Shirika la Kimataifa ya Maendeleo ya Uingereza (DFID), Shirika la Kimataifa la Kijerumani la Ushirikiano wa Kimataifa (GIZ), Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden (SNAO), Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), Benki ya Dunia (WB) na washirika wetu wengine ambao wametoa mchango mkubwa katika ofisi yangu na kuzifanya kazi za ukaguzi ziwe za kitaalam zaidi kwa kutoa fedha kwa ajili ya kujenga uwezo kwa wafanyakazi na kutoa vitendea kazi.

Wakati nawasilisha taarifa zangu za ukaguzi mwezi Machi 2017, Mheshimiwa Rais alimuagiza Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba naziwasilisha taarifa hizo pia kwa Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Maafisa Tawala wa Mikoa. Kutohana na juhudhi za Waziri Mkuu mkutano uliandaliwa na niliwasilisha taarifa hizo kama ilivyoagizwa.

Aidha, kutokana na mukutano huo nimeona kuwa kuna juhudii za makusudi zinazofanywa na watekeleza miradi ambapo ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa zangu umeboreka.

Mwisho, natoa shukrani zangu kwa mchapishaji wa taarifa hii kwa kuniwezesha kuitoa kwa wakati.

## MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU

### i. Utangulizi

Sehemu hii ya ripoti inatoa maelezo ya jumla ya matokeo ya ukaguzi wa taarifa za hesabu yanayotakiwa kuzingatiwa kwa umakini na Serikali, Bunge, Maafisa Masuuli na Wadau wengine wa miradi ya maendeleo.

Taarifa hii inajumuisha muhtasari wa mambo muhimu yaliyotokana na ukaguzi ambapo taarifa zake kwa ujumla zimeelezwa katika barua ya mapungufu na katika taarifa ya ukaguzi inapelekwa kwa watekelezaji wa miradi. Katika ripoti hii tumewasilisha mambo ambayo tumeona ni ya muhimu kuletwa kwa Serikali, wasimamizi wa taasisi pamoja na Umma.

Aidha, nimegundua mapungufu katika masuala ya usimamizi wa fedha na bajeti, mifumo ya ndani, na usimamizi wa kanuni na sheria. Mapungufu haya yanahitaji kufanyiwa kazi na watekeleza miradi ili kuboresha utendaji katika siku zijazo.

### ii. Hoja Muhimu Zilizojitokeza Wakati wa Ukaguzi

Aya hii inaelezea hoja muhimu zilizojitokeza kwenye ukaguzi zinazohitaji kufanyiwa kazi kipekee kama mapendekezo yanavyoonesha katika aya ya 6.2 ya taarifa hii.

#### a) Kutolipwa Fidia kwa Watu Walioathiriwa na Miradi Sh.Tz. bilioni 11.9

Nimeibaini kuwa watu walioathiriwa na utekelezaji wa miradi mitatu; Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP II), Programu ya Msada wa Sekta ya Usafiri (TSSP) na Miradi wa Barabara ya Arusha-Taveta / Holili-Voi hawajalipwa fidia ya jumla ya Sh.Tz. 11,870,767,751 (**kiambatisho 1(i)**).

- b) Kutolipa Gharama za Uchangiaji Kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na “Global Fund” Sh.Tz. bilioni 61.4**
- Ukaguzi wangu umegundua kuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria, UKIMWI na Kifua Kikuu (Global Fund) wameshindwa kuchangia jumla ya Sh.Tz. 61,441,762,383.76 kwenda Bohari ya Dawa (MSD). Kiasi hiki kinatokana na kutochangia asilimia 5.6 kwa ajili ya gharama za uhifadhi na usambazaji wa dawa na vifaa-tiba kama inavyoelekezwa na mkataba wa makubaliano baina yao (**kiambatisho 1(ii)**).
- c) Malipo ya Riba Iliyotokana na Adhabu kwa Kuchelewesha Malipo ya Wakandarasi Sh.Tz. bilioni 3.9**
- Ilibainika kuwa jumla ya Sh.Tz. 3,889,404,110 zililipwa kama riba kutokana na adhabu ya kutolipa madai ya wakandarasi kwa wakati. Malipo haya yalihuisha miradi ya Programu ya Msada katika Sekta ya Barabara Awamu ya Kwanza (RSSP I), RSSP II na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji awamu ya pili (WSDP II). Aidha nilifahamishwa kwamba malipo ya wakandarasi yalishindikana kufanyika kwa wakati kutokana na Hazina kutopeleka fedha za miradi kwa wakati (**kiambatisho 1(iii)**).
- d) Fedha za Ushuru wa Mafuta na Usafirishaji Zilizokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania Zimepelekwa Pungufu Kwenye Akaunti ya Mfuko wa Barabara Sh.Tz. bilioni 14.8**
- Kwa kawaida Mamlaka ya Mapato Tanzania hukusanya fedha za ushuru wa mafuta na usafirishaji kisha huzihamishia kwenye Akunti ya Mfuko wa Barabara kupitia Wizara ya Fedha na Mipango.

Ukaguzi wangu umebaini kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania haikupeleka kiasi cha Sh.Tz. 14,828,686,613.55 kwenye Akaunti ya Mfuko wa Barabara. Hii inatokana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya kiasi cha Sh.Tz. 755,688,604,775.57 na kupeleka kiasi pungufu kwenye

akaunti ya mfuko wa barabara ambacho ni Sh.Tz. 740,859,918,162.02.

e) **Kutorejeshwa kwa Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Ambazo Zililipwa kwa Kaya Zisizostahili Sh.Tz. milioni 593.3**

Iligundulika kuwa jumla ya Sh.Tz. 593,320,300 zililipwa kwa kaya zisizostahili kutoka kwenye maeneo 13 ya mamlaka ya mradi (PAA). Aidha, kaya hizo bado hazijarejesha kiasi hicho cha fedha kinyume na Ibara 1.7 ya Muongozo wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (**kiambatisho 1(iv)**).

f) **Matumizi Yaliyofanyika Nje ya Bajeti Iliyoidhinishwa Sh.Tz. bilioni 4.3**

Watekeleza miradi 46 walitumia jumla ya Sh.Tz. 4,296,264,090.79 kufanya shughuli ambazo ziliwuwa nje ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kufanya matumizi nje ya shughuli zilizoidhinishwa na bajeti kulisababisha kutokamilika kwa baadhi ya shughuli za miradi hiyo zilizokuwa kwenye mpango (**kiambatisho 1(v)**).

g) **Kutolewa Fedha Pungufu kwa Ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Sh.Tz. bilioni 274. 6**

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa watekeleza miradi 257 sawa na asilimia 35 ya watekeleza miradi wote walipokea fedha pungufu kwa Sh.Tz. 274,647,963,420.86 kinyume na bajeti iliyoidhinishwa. Hazina na baadhi ya Wafadhili walichelewa kutoa fedha hizi kutoana na sababu mbalimbali ikiwemo upelekeji wa taarifa za fedha zenye mapungufu kwenda kwa wafadhili kinyume na makubaliano. Aidha, utoaji wa fedha pungufu hupelekea miradi hiyo kutokukamilika kwa wakati na kuwa kwenye uwezekano wa kukabiliwa na ongezeko la gharama za miradi (**viambatisho 1(vi) na 1(vii)**).

**h) Malipo Yaliyofanyika na Viambatisho Pungufu Sh.Tz. bilioni 8.7**

Nilibaini uwepo wa malipo ya jumla ya Sh.Tz. 7,248,937,125.89 ambayo yalifanywa na watekeleza miradi 163 bila kuwa na viambatisho vya kutosha. Aidha, nilishindwa kupata hati za malipo kwa matumizi ya Sh.Tz. 1,464,506,137.88 ambazo zililipwa na watekeleza miradi 21. Hivyo, kwa ujumla nimeshindwa kutambua uhalali wa malipo ya Sh.Tz. 8,713,443,263.77 kutokana na kukosekana kwa nyaraka za viambatisho (**viambatisho 1(viii) na 1(ix)**).

**i) Kutokudai Marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) Sh.Tz. bilioni 1.6**

Niligundua kuwa watekeleza miradi 16 wameshindwa kudai kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) jumla ya Sh.Tz. 1,588,581,132.46 kutokana na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kinyume na makubaliano yaliyosainiwa kati ya Serikali na Wafadhili (**kiambatisho 1(x)**).

**j) Malipo Yaliyofanyika Kwenye Vifungu vya Matumizi Visivyo Sahihi Sh.Tz. bilioni 1.1**

Nimebaini kuwa jumla ya Sh.Tz. 1,091,406,059 zililipwa kupitia vifungu vya matumizi ambavyo siyo sahihi, kinyume na Agizo Na.23 (1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa (LGF) 2009. Kuchanganya vifungu vya matumizi kunasababisha baadhi ya vifungu kupungukiwa na fedha, hivyo kushindwa kutumika kufanya kazi zilizokusudiwa (**kiambatisho 1(xi)**).

**iii. Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi Yatokanayo na Ripoti za Kaguzi za Miaka Iliyopita**

Imeonekana kuwa Maafisa Masuuli na watendaji wakuu wa taasisi zinazotekeleza miradi ya maendeleo hawatekelezi kikamilifu mapendekezo yangu; ambapo, mapendekezo 2,720, sawa na asilimia 35 ya mapendekezo yangu ya mwaka uliopita, hayakutekelezwa kama ilivyooneshwa kwa undani kwenye Sura ya 2.1 ya ripoti hii.

#### **iv. Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi Zilizotolewa**

Nimekagua jumla ya miradi ya maendeleo 742 ndani ya mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2017. Idadi hiyo inajumuisha miradi ya maendeleo 664 kutoka katika ripoti kubwa tano, yaani Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP), Mfuko wa Uchangiaji wa Sekta ya Afya (HBF), Mfuko wa Barabara (RF), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) ikiwa na idadi ya hati 56, 181, 177, 70 na 180 mtawalia. Aidha miradi mingine ilikuwa na hati 78.

Nimetoa jumla ya hati za ukaguzi 742 kwa mwaka wa fedha 2016/2017; ambapo hati 697, sawa na asilimia 94 ya hati zote zilizotolewa zilipata hati zinazoridhisha; hati 44, sawa na asilimia 6, zilipata hati zenyenye mashaka. Hati chafu ilitolewa kwa halmashauri moja; hakuna hati mbaya iliyotolewa. Aidha, sijagundua mabadiliko makubwa kwenye hati za ukaguzi zilizotolewa katika mwaka huu kulinganisha na mwaka wa fedha uliopita.

Hata hivyo, hati zenyenye shaka zimejitokeza kwa wingi kwenye mradi wa Mfuko Mkuu wa Afya na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji zikiwa na jumla ya hati zenyenye shaka 14 na 13 mtawalia.

## SURA YA KWANZA

### USULI NA TAARIFA ZA UJUMLA

#### **1.0 Utangulizi**

Ukaguzi wa Kisheria wa taarifa za fedha za miradi ya maendeleo inayotekelawa nchini kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2017 umekamilika. Ukaguzi huu umejumuisha miradi mitano mikubwa ambayo ni ASDP, HBF, RF, TASAF na WSDP, aidha, ilijumuisha miradi mingineyo inayofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Umoja wa Mataifa na makubaliano ya kifedha baina ya JMT na nchi nyingine kupitia taasisi zao.

Ofisi yangu ilipanga kukagua jumla ya miradi 768 ikijumuisha miradi mikubwa mitano na miradi mingineyo. Kufikia tarehe 31 Machi 2018, nilimaliza ukaguzi wa miradi 742 kama ifuatavyo; ASDP, HBF, RF, TASAF, WSDP na miradi mingineyo kwa idadi ya 56, 181, 177, 70, 180 na 78 mtawalia, ilhali ukaguzi wa miradi 26 ukiwa unaendelea. Hata hivyo, nimefanikiwa kumaliza ukaguzi wa miradi 31 iliyokuwa haijakamilika kwenye mwaka wa fedha 2015/2016

Muhtasari wa mambo muhimu yaliyotokana na ukaguzi yameonyeshwa katika taarifa hii ya jumla. Aidha, taarifa kamili zilipelekwa kwa uongozi wa kila mkaguliwa anayesimamia utekelezaji wa mradi na wadau wengine wanaohusika na miradi.

#### **1.1 Mamlaka na Umuhimu wa Ukaguzi**

Kutokana na Ibara ya 143 ya Katiba ya JMT, ninapaswa kukagua taarifa zote za hesabu za fedha katika ofisi zote za Umma, Mahakama na Mamlaka zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Rais ambaye atahakikisha zinawasilishwa mbele ya Bunge.

Katika kutimiza wajibu huu, kifungu Na.10 cha Sheria Na. 11 ya Ukagazi wa Umma ya mwaka 2008 kinanitaka kujiridhisha kwamba fedha zote zinazotolewa zinatumika kulingana na malengo yaliyokusudiwa.

**1.2 Wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

Wajibu wangu kama Mkaguzi wa Hesabu ni kutoa maoni ya ukagazi kuhusu taarifa za fedha za miradi ya maendeleo kutokana na ukagazi nilioufanya. Nilifanya ukaguzi kulingana na viwango vya kimataifa vinavyosimamia ukaguzi katika Taasisi za Umma za Ukagazi (ISSAIs), mkataba wa makubaliano na taratibu nyingine nilizoona zinafaa.

Aidha, kifungu Na. 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kinanitaka nijiridhishe kama taarifa za hesabu zimeandaliwa kwa misingi ya viwango vya kihasibu, na tahadhari za kutosha zimechukuliwa kulinda ukusanyaji wa mapato, stakabadhi, uhifadhi, uuzwaji, uhamasishwaji pamoja na matumizi sahihi wa mali ya umma. Na, ni wajibu wangu kuona kuwa sheria, kanuni maelekezo na maagizo yanafuatwa katika matumizi ya fedha za umma, na kwamba, yameidhinishwa ipasavyo.

Zaidi, kifungu 48(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 7 ya mwaka 2011 kinanitaka katika ripoti yangu nitoe tathmini kama taarifa nilizokagua zinakidhi matakwa ya sheria na kanuni zake.

**1.3 Muundo wa Kazi za Ukaguzi katika Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Ripoti hii inatoa kwa muhtasari matokeo ya mwisho ya zoezi la ukaguzi ambalo lilifanywa na ofisi yangu nchini kote katika mwaka huu. Ili ofisi yangu iweze kushughulikia kikamilifu kazi hii kubwa ya kukagua miradi ya maendeleo iliyoteklezwa na Halmashauri zote nchini, wakala wa serikali, na wabia wengine, nimeunda ofisi katika mikoa yote Tanzania Bara ili kurahisisha utendaji. Ofisi hizo zinaongozwa na Wakaguzi Wakuu wa Nje. Aidha, nafanya kaguzi zangu kwa kuzingatia

viashiria hatarishi (*risk based audit*) zinazotekelze wa kwa kutumia teknolojia maalum ya kompyuta (*Computer Assisted Audit Techniques (CAATs)*).

Wakati mwingine niliazima wakagazi kutoka nje ya ofisi yangu ili kusaidia ukagazi kama ninavyoruhusiwa na Sheria Namba 33 ya Ukagazi wa Umma ambayo inanipa mamlaka ya kumthibitisha mkagazi yeyote mwenye sifa na aliyesajiliwa na Bodi ya Uhasibu nchini chini ya Sheria Namba 33 ya Usajili wa Wahasibu Na Wakagazi ya mwaka 1972 (iliyorekebishwa mwaka 1995).

## **1.4 Mawanda na Viwango vya Ukagazi Vinavyotumika**

### **1.4.1 Mawanda ya Ukagazi**

Mawanda ya Ukagazi yalihuisha tathmini ya ufanisi wa mifumo ya kihasibu pamoja na udhibiti wa ndani wa shughuli, upimaji na uthibitishaji wa viambatisho vya nyaraka za fedha, taarifa za utekelezaji na taratibu nyingine za kikagazi zilizopaswa kuzingatiwa ili kupatikana kwa taarifa ya ukagazi. Kagazi zimefanyika kwa kuzingatia vihatarishi na uzito wa tatizo lilioibuliwa. Hivyo, hoja za ukagazi zimetokana na taarifa zilizopokelewa kwa ajili ya kukaguliwa.

Lengo kuu la kufanya ukagazi ni kumsaidia Mdhibiti na Mkagazi Mkuu kutoa maoni yake kwa uhuru kuhusiana na taarifa za fedha za miradi ya maendeleo zilizoandaliwa na kuwasilishwa kwa ajili ya kuzikagua. Vilevile, kuona kama zimeandaliwa kwa kuzingatia miongozo ya uandaaji wa taarifa za fedha wa kimataifa.

### **1.4.2 Viwango vya Ukagazi Vinavyotumika**

Ofisi ya Taifa ya Ukagazi wa Hesabu za Serikali (NAOT) ni mwanachama wa Jumuiya Kuu ya Kimataifa ya Asasi Kuu za Ukagazi wa Hesabu (INTOSAI) na Jumuiya ya Afrika ya Asasi Kuu za Ukagazi kwa Nchi Zinazozungumza Lugha ya Kiingereza (AFROSAI-E). Hivyo basi, taratibu zilizotumika zimezingatia

Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi kama vile ISSAI na ISA vinavyotolewa na INTOSAI na IFAC mtawalia.

Viwango hivi vinanitaka kuzingatia maadili katika kuandaa na kutekeleza ukaguzi wangu ili kupata uhakika kwamba taarifa za hesabu zipo sahihi na hazina makosa makubwa. Hata hivyo, taarifa za kifedha za Miradi ya Maendeleo ziwe zimeandaliwa kwa mujibu wa makubaliano baina ya wabia yaliyosainiwa.

### **1.5 Wajibu wa Maafisa Masuuli**

Kifungu Na. 25(4) cha Sheria ya Fedha Na. 6 ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) kinamtaka Afisa Masuuli kuandaa taarifa za fedha zilizo sahihi kwa kila kipindi cha mwaka kuonyesha mapato na matumizi ya mradi hadi kufikia mwisho wa mwaka.

Aidha, maagizo namba 11, 14 na 31 (1) ya Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya 2009, na Mkataba wa Makubaliano (MoU) baina ya watekelezaji wa Mradi na wadau wa maendeleo yanawataka wahusike kuhakikisha kwamba kumbukumbu sahihi za kihasibu za miradi zinatunzwa vizuri; na mfumo wa udhibiti wa ndani udhibitiwe.

## SURA YA PILI

### HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA RIPOTI ZA KAGUZI ZA MIAKA YA NYUMA

#### 2.0 Utangulizi

Sura hii inalenga kutoa taarifa ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za kaguzi za miaka ya nyuma. Pia, ni muhtasari wa masuala ya kifedha na yasiyo ya kifedha yaliyoibuliwa katika kila ripoti ya mradi yaliyokuwa yametekelawa kwa sehemu au hayajatekelawa kabisa. Mapendekezo ya ukaguzi yanayotolewa kwa wakaguliwa hulenga kuwezesha kufanya maboresho na kurekebisha kasoro zilizoonekana wakati wa ukaguzi wa taarifa za hesabu.

#### 2.1 Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi Zilizopita

Kama inavyoonekana kwenye Kiambatisho Na.3, kulikuwa na mapendekezo ambayo hayajatekelawa kwenye Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2017. Kati ya hayo, 2,220 sawa na asilimia 29 yalitekelawa; 1,325 sawa na asilimia 17 yanaendelea kutekelawa; 2,720 sawa na asilimia 35 hayakutekelawa; na 1,475 sawa na asilimia 19 yamefutika kutokana na mazingira na wakati.

Ingawa utekelezaji wa mapendekezo yangu umeboreka kidogo kwa asilimia 5 ingawa kwa ujumla utekelezaji wa mapendekezo yangu bado hauridhishi ambapo asilimia 35 ya mapendekezo yangu hayajatekelawa ikilinganishwa na asilimia 40 ya mwaka uliopita. Aidha, utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi bado hauridhishi kutokana na idadi kubwa ya mapendekezo yaliyopita. Uchambuzi unaonesha kwamba mapendekezo 145 kati ya 408 ya Programu ya Maendeleo Sekta ya Kilimo ambayo ni sawa na asilimia 36 bado hayajatekelawa; mapendekezo 728 kati ya 2,043 ya Mfuko wa Barabara ambayo ni sawa na asilimia 36 hayajatekelawa. Aidha, mapendekezo 1,014 kati ya 2,437 ya Mfuko wa Uchangiaji Sekta ya Afya ambayo ni sawa na

asilimia 42 bado hayajatekelezwa; mapendekezo 678 kati ya 2,058 ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo ni sawa na asilimia 33 bado hayajatekelezwa; na mapendekezo 84 kati ya 424 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ambayo ni sawa na asilimia 20 bado hayajatekelezwa. Zaidi ya hayo, mapendekezo 71 kati ya 370 ya Miradi Mingineyo ambayo ni asilimia 19 bado hayajatekelezwa. Rejea jedwali hapa chini kwa maelezo zaidi:

**Jedwali Na. 1: Utekelezaji wa Mapendekezo Katika Ripoti za Kaguzi za Miaka ya Nyuma**

Jina la Mradi	Mapendek ezo ya Miaka ya Nyuma	Mapende kezo Yaliyote kelezwa	Mapendekez o Yanayoendel ea kutekelezwa	Mapendek ezo ambayo hayajateke lezwa	Mapendekezo yaliyofutika kutokana na Mazingira na Wakati
Programmu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo	408	76	87	145	100
Mfuko wa Barabara	2,043	566	309	728	440
Mfuko wa Uchangiaji wa Afya	2,437	651	332	1014	440
Mfuko wa Maendeleo ya Jamii	424	221	74	84	45
Programmu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji	2,058	517	436	678	427
Miradi mingineyo	370	189	87	71	23
<b>Jumla</b>	<b>7,740</b>	<b>2,220</b>	<b>1,325</b>	<b>2,720</b>	<b>1,475</b>
<b>Asilimia</b>	<b>100</b>	<b>29</b>	<b>17</b>	<b>35</b>	<b>19</b>

*Chanzo: Ripoti za Ukaguzi za miaka iliyopita*

Kwa hiyo, nasisitiza kuwa watekeleza miradi wahakikishe wanayafanya kazi ili kuepusha kujirudiarudia kwa mapungufu hayo, hatimaye kuboresha uwajibikaji katika matumizi ya fedha zilizopokelewa. Aidha, nashauri kuwa mapendekezo yote ambayo yametekelawa kwa sehemu au

hayajatekelezwa kabisa yatekelezwe kwa wakati ili kuboresha usimamizi wa miradi hiyo.

## SURA YA TATU

### AINA NA MWENENDO WA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

#### 3.0 Utangulizi

Katika kutimiza wajibu wangu wa kisheria, nina jukumu la kuwahakikishia wadau wote wa miradi ya maendeleo kuwa taarifa za fedha za miradi ya maendeleo yam waka unaoishia tarehe 30 Juni, 2017 zimeandaliwa kulingana na taratibu na miongozo sahihi ya kutengenezea hesabu.

Hati ya ukaguzi inachukuliwa kama chombo muhimu wakati wa kuwasilisha taarifa ya kifedha kwa walengwa wanaotumia taarifa hizi. Katika sekta ya umma, inakusudiwa kulishauri Bunge na watumiaji wengine wa taarifa za Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kama taarifa za fedha zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vinavyoendana na IPSAS na kwa namna inavyotakiwa chini ya Kifungu cha 25(4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) na Agizo namba 11-14 ya Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009, na mkataba wa makubaliano kati ya watekelezaji na wadau wa maendeleo, ambayo inawataka kuhakikisha kuwa usimamizi wa kumbukumbu za uhasibu na mfumo wa udhibiti wa ndani unaimarika.

Kwa upande wa miradi ya maendeleo, nimetao aina kuu tatu za hati kutokana na kukagua vitabu vya hesabu, mifumo ya udhibiti wa ndani, na uziangatiaji wa taratibu. Nimetao jumla ya hati 742 kutokana na ukaguzi wa vitabu vya hesabu, hati 35 kutokana na ukaguzi wa mifumo ya udhibiti wa ndani, na hati 6 kutokana na ukaguzi wa uziangatiaji wa taratibu.

Aidha sijabaini mapungufu makubwa kiasi cha kutolea taarifa katika hati hizo 41 za mifumo ya udhibiti wa ndani na uzingatiaji wa taratibu, ambapo zimetokana na ukaguzi wa miradi iliyofadhiliwa na Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia

Watoto na Elimu na Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na Malaria, UKIMWI na Kifua Kikuu.

### 3.1 Aina za Hati za Ukaguzi

Katika mwaka huu wa fedha nimekagua jumla ya miradi ya maendeleo 742 na kutoa aina tatu za hati za ukaguzi ambazo ni hati inayoridhisha, hati isiyoridhisha na hati mbaya kama inavyoonekana kwenye jedwali namba mbili hapo chini:

**Jedwali Na 2: Muhtasari wa Hati za Ukaguzi Zilizotolewa**

Jina la Miradi	Hati za Ukaguzi				
	Hati Zinazoridh isha	Hati Zenye Shaka	Hati Zisizoridh isha	Hati Mbaya	Jumla
Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo	55	1			56
Mfuko wa Uchangiaji wa Afya	167	14			181
Mfuko wa Bara Bara	169	8			177
Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania	66	4			70
Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji	166	13	1		180
Miradi Mingineyo	74	4			78
<b>Jumla Kuu</b>	<b>697</b>	<b>44</b>	<b>1</b>		<b>742</b>

Chanzo: Taarifa za Ukaguzi za miradi ya maendeleo za unaoishia 30 Juni 2017

#### 3.1.1 Hati Inayoridhisha

Aina hii ya hati (kama ilivyoelezewa katika ISSAI 1700.16) hutolewa wakati taarifa za fedha zilizowasilishwa na kukaguliwa zinakutwa hazina makosa mengi na zimezingatia matakwa ya viwango vya Kimataifa vya Uhасибу katika Sekta ya Umma ikihusisha uzingatiwaji wa Sheria na Kanuni.

Jumla ya hati zinazoridhisha 697 sawa na asilimia 94 zilitolewa kwenye Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Mfuko wa Pamoja wa Afya, Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na Miradi Mingineyo zikiwa ni 55, 167, 169, 66,166 na 74 mtawalia, ikimaanisha kwamba hesabu zilizokaguliwa

hazikuwa na matatizo sana. Kama inavoonekana kwenye aya ya 3.2 hali ya hati hizo imeboreka kidogo kwa asilimia 3 ikilinganishwa na mwaka 2015/2016 ambapo kulikuwa na hati 725 zinazoridhisha sawa na asilimia 91 ya hati zote zilizotolewa (**Kiambatisho 4(i) na 4(ii)**).

### 3.1.2 Hati Yenye Mashaka

Hati yenye mashaka (Kama ilivyoelezwa katika ISSAI 1705.7) hutolewa wakati: (a) Mkaguzi anapopata ushahidi na vielelezo vya kutosha kujiridhisha kwamba mapungufu yaliyojitokeza ni makubwa lakini hayana athari kwenye hesabu kwa ujumla; (b) Mkaguzi hakuweza kupata vielelezo na ushahidi wa kutosha lakini amejiridhisha kwamba athari ya kukosekana kwa vielelezo hivyo siyo kubwa kwenye hesabu zilizokaguliwa. Kwa hali hiyo, hati yenye shaka inaonyesha kuwa taarifa za fedha zilizowasilishwa ni sahihi isipokuwa kwa madhara yatokanayo na masuala halisi ya kiukaguzi yaliyogunduliwa.

Aidha, jumla ya hati za mashaka 44 sawa na asilimia 6 ya hati za ukaguzi zilitolewa kwa miradi ya maendeleo iliyokaguliwa ya ASDP, HBF, RF, TASAF, WSDP, na miradi mingineyo kwa 1, 14, 8, 4, 13 na 4 mtawalia. Katika mradi wa afya nimegundua hati 14 zisidhoridhisha ambazo ni sawa na asilimia 32 ya hati zote zisidhoridhisha. Idadi kubwa ya miradi hii imepata hati zisizoridhisha kutokana na malipo mengi kukosa viambatisho pamoja na vitabu vya hesabu kuandaliwa vikiwa na makosa mengi ambayo hayakurekebishwa kwa wakati mpaka ukaguzi ulipomalizika (**kiambatisho 4(iii)**).

Kuwapo kwa matumizi yasiyo na viambatisho kunaonesha kuna tatizo kubwa katika udhibiti wa matumizi na utunzaji wa kumbukumbu za hesabu katika miradi hiyo. Hii inaweza kusababisha malengo kusudiwa ya miradi kutofikiwa, hivyo Serikali na Watekeleza miradi wanatakiwa kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba matumizi ya miradi yanakuwa na viambatisho stahiki.

### **3.1.3 Hati Isiyoridhisha**

Hati isiyoridhisha (Kama ilivyoelezewa kwenye ISSAI 1705.8) hutolewa inapogundulika kuwa taarifa za fedha kwa kiasi kikubwa si sahihi zinapoangaliwa katika ujumla wake; na kwamba, hazikuandaliwa kwa kuzingatia mifumo ya kihasibu. Maelezo ya hati isiyoridhisha huwa wazi ambapo inaeleza wazi kwamba taarifa za fedha hazikuzingatia na kufuata mfumo wa uhasibu na viwango vyta Kimataifa vya Uhasibu katika sekta ya Umma.

Katika ukaguzi huu nimetoa hati moja isiyoridhisha kwa Halmashauri ya Wilaya ya Makete kwa mradi wa programmu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

### **3.1.4 Hati Mbaya**

Hati mbaya (kama ilivyoelezewa katika ISSAI 1705.9&10) inaweza kusababishwa na kukosekana kwa uhuru au ufinyu mkubwa wa mawanda ya ukaguzi ama kwa makusudi au la. Mkaguliwa kukataa kutoa ushahidi na taarifa kwa mkaguzi katika maeneo muhimu kwenye taarifa za fedha na panapokuwa na mashaka makubwa katika uendeshaji wa shughuli za mkaguliwa. Katika mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2017 sijatoa hati mbaya kwa mtekelezaji yejote wa miradi ya maendeleo.

## **3.2 Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi**

Nawasilisha mchanganuo wa hati za ukaguzi kwa muda wa miaka miwili ya nyuma. Aidha, hakuna mabadiliko makubwa yaliyoonekana katika hati za ukaguzi zilizotolewa ikilinganishwa na mwaka 2015/2016 kama inavyoonekana kwenye jedwali namba 3 hapo chini:

**Jedwali Na. 3: Mwelekeo wa hoja za ukaguzi**

Mwaka wa Fedha	Hati zilizotolewa						Jumla	
	Zinazoridhisha		Zenye shaka		Zisizoridhisha			
	No.	%	No.	%	No.	%		
2016/2017	697	94	44	6	1	0.13	742	
2015/2016	725	91	71	9	1	0.13	797	
2014/2015	739	92	60	8	-	-	799	

*Chanzo: Taarifa za Ukaguzi wa Miradi ya Mendeleo za miaka ya nyuma*

Jedwali hapo juu linaonesha uborekaji katika hati zilizotolewa ambapo zinazoridhisha zimeongezeka kwa asilimia 3 na hati zenye shaka zimepungua kwa asilimia 3 pia. Aidha hakuna mabadiliko kwenye hati zisizoridhisha ambapo zimebakia kuwa asilimia 0.13 kwa miaka miwili mfululizo.

Kama ilivoelezewa kwenye aya za 3.1.2 na 3.1.3, kwamba nimetoa hati 44 zenye shaka na hati 1 isiyoridhisha zilizotokana na makosa yasiyorekebishwa kwenye ufungaji wa hesabu pamoja na malipo yenyе viambatanisho pungufu.

## SURA YA NNE

### UTENDAJI WA KIFEDHA WA MIRADI

#### 4.0 Utangulizi

Sura hii inatoa mchanganuo wa kina wa utendaji wa kifedha katika miradi ya maendeleo ikiwemo Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP), Mfuko wa Uchangiaji wa Afya (HBF), Mfuko wa Barabara (RF), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) pamoja na miradi mingine ya maendeleo. Inatoa mchanganuo wa kiasi cha fedha kilichotumwa na kutumiwa na watekelezaji wa miradi. Undani wa utendaji wa kifedha kwa kila mradi ni kama inavyooneshwu kwenye **Kiambatisho 5.**

#### 4.1 Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP)

##### 4.1.1 Utangulizi

Programu hii inajumuisha mipango ya kuendeleza kilimo kitaifa na kisekta inayofadhiliwa kwa pamoja na Serikali ya Tanzania na Washirika wa Maendeleo kupitia Mfuko wa pamoja wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ambao ultanguliwa na Programu ya kusaidia Sekta ya Kilimo (ASSP) na Programu ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADP).

Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) inatekelezwa na Wizara na Serikali za Mitaa na malengo yake yamewekwa chini ya Mfumo wa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDS).

##### 4.1.2 Ufadhilli

Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) inafadhiliwa na michango na mikopo kutoka Washirika wa Maendeleo kupitia Ubalozi wa Ireland, Shirika la Kimaendeleo la Kimataifa (IDA), Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD) na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA). Fedha zinapokelewa kupitia akaunti kuu ya mradi iliyoko Hazina na kisha kupelekwa kwa watekeleza miradi

Programu ilianza mwaka kwa salio anzia la kiasi cha Dola za Kimerakani (DK) 4,218,560.28 (Sh.Tz. 9,361,194,080.05) katika akaunti ya mfuko mkuu na haikupokea fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo. Kiasi cha DK 344,849.35 (Sh.Tz. 765,237,777.69) kilihamishwa na kubaki salio ishia la DK 3,873,710.93(Sh.Tz. 8,595,956,302.36).

Wakati mfuko mkuu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo awamu ya pili wa Matokeo Makubwa Sasa ulikuwa na salio anzia DK 611,972.01 (Sh.Tz. 1,357,996,182.80) na kupokea kiasi cha DK 351,312.23 (Sh.Tz. 779,579,228.33) kutoka Shirika la Maendeleo la Kimataifa. Jumla ya DK 361,287.48 (Sh.Tz. 801,714,801.85) na DK 157,537.47 (Sh.Tz. 349,583,444.03) zilitumwa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na kubakiwa na salio la DK 444,459.29 (Sh.Tz. 986,277,165.24) Jedwali hapo chini linaonesha.

**Jedwali Na. 4: Jumla ya Fedha za Mpango wa Maendeleo Sekta ya Kilimo Zilizopokelewa na Kuhamishwa**

Maeleo	Kiasi (DK)	
	Akaunti ya Mfuko mkuu wa ASDP	Akaunti ya Mfuko mkuu wa ASDP II-Matokeo Makubwa Sasa
Salio anzia 1 Julai 2016	4,218,560.28	611,972.01
Fedha iliyopokelewa:		
Shirika la Maendeleo la Kimataifa	-	351,312.23
<b>Jumla ya fedha zilizopokelewa</b>	<b>4,218,560.28</b>	<b>963,284.24</b>
Fedha zilizohamishwa		
Wizara ya Maji na Umwagiliaji	-	157,537.47
Wizara ya Kilimo	204,958.14	361,287.48
Fedha zilizorudishwa kutoka Shirika la Maendeleo la Kimataifa	139,891.21	-
<b>Jumla ya fedha zilizohamishwa</b>	<b>344,849.35</b>	<b>518,824.95</b>
<b>Salio Ishia 30 Juni 2017</b>	<b>3,873,710.93</b>	<b>444,459.29</b>

*Chanzo: Taarifa ya fedha Mfuko mkuu wa Mpango wa Maendeleo ya sekta ya Kilimo ya 30 June 2017.*

#### **4.1.3 Fedha za Mradi kwa Serikali za Mitaa**

Mamlaka za serikali za mitaa zilikuwa na jumla ya Sh.Tz. 14,496,390,704.20 kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo katika Sekta ya Kilimo; ambapo Sh.Tz. 13,348,387,781.20 ilikuwa salio anzia na Sh.Tz. 1,148,002,923 zilipokelewa mwaka huu kwa ajili utekelezaji wa miradi iliyopangwa. Aidha Sh.Tz. 9,177,271,288 zilitumika na kubaki na salio ishia la Sh.Tz. 5,319,119,416.20 ambalo ni sawa na asilimia 37 ya fedha iliyokuwepo kwa ajili ya kukamilisha kazi zilizopangwa.

### **4.2 Fedha za Mfuko wa Uchangiaji wa Afya (HBF)**

#### **4.2.1 Utangulizi**

Washiriki wa Mfuko wa Uchangiaji wa Afya nchini huchangiwa fedha na wadau wa kupitia akaunti maalum katika Benki Kuu ya Tanzania na baadaye kuhamisha fedha hizo kwenda Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, OR-TAMISEMI na SM kwa kutoa fedha kwa mgawo wa robo mwaka kupitia Akaunti kuu ya Hazina. Ufadhilli hufuata utaratibu wa kawaida wa Serikali ya Tanzania (JMT) ambapo fedha za Washirika wa maendeleo hujumuishwa katika bajeti kuu.

#### **4.2.2 Ufadhilli**

Mfuko wa Uchangiaji wa Afya ulianza mwaka 2016/2017 ukiwa na salio anzia la DK 15,547,235.25 (Sh.Tz. 33,704,866,845.71) na kupokea kiasi cha DK 74,682,274.4 (Sh.Tz. 161,616,252,402.8) kisha kupeleka jumla ya DK 68,008,853.98 (Sh.Tz. 148,705,727,340) kwa watekeleza miradi 181. Mpaka kufikia mwisho wa mwaka, Mfuko ulibaki na bakaa ishia la DK 22,220,655.67 (Sh.Tz. 49,308,745,964.51). Wachangiaji wakuu katika mwaka huu wa fedha ni Denmark (asilimia 12) Ireland (asilimia12), Uswisi(asilimia8.2), KOICA (asilimia1.34), UNICEF (asilimia1.34), IDA (asilimia46) na Canada (asilimia 19) ya jumla ya fedha yote iliyochangwa. Jedwali hapo chini linaonesha mchanganuo huu:

**Jedwali Na. 5: Jumla ya Fedha Zilizokusanya Kutumwa Mfuko wa Uchangiaji wa Afya**

Maelezo	Kiasi (DK)	Michango kwa asilimia
Salio anzia 1 Julai 2016	15,547,235.25	
Mapokezi ya Fedha		
Denmark	8,724,129.27	12
Ireland	8,981,600	12
Uswisi	6,105,000	8.2
Shirika la Misaada la Kijapani (KOICA)	1,000,000	1.34
Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu na Watoto (UNICEF)	1,000,000	1.34
Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA)	34,671,730.70	46
Canada	14,137,472.79	19
Kurudishwa kwa fedha za ziada	62,341.64	
Jumla ya fedha iliyopokelewa	74,682,274.40	
<b>Jumla ya Fedha iliyopo</b>	<b>90,229,509.65</b>	
Fedha zilizohamishwa		
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto	67,879,547.02	
OR-TAMISEMI	129,306.96	
Jumla ya fedha zilizohamishwa	68,008,853.98	
<b>Salio ishia 30 Juni 2017</b>	<b>22,220,655.67</b>	

*Chanzo: Taarifa ya fedha ya Mfuko wa Uchangiaji wa Afya inayoishia 30 Juni 2017*

**4.2.3 Fedha zilizotumwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, OR-TAMISEMI na SM**

Jumla ya Sh.Tz. 8,768,477,000, Sh.Tz. 30,085,677,840; na Sh. 105,827,586,360 ilipokelewa na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, OR-TAMISEMI na SM mtawalia kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Afya; ambapo Sh.Tz. 7,357,570,608, Sh.Tz. 6,192,407,085.06 na Sh.Tz. 115,546,902,047.11 zilitumika na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto, OR-TAMISEMI, SM kama jedwali linavyoonesha hapa chini:

Jedwali Na. 6: Fedha zilizotumwa kwa Watekelezaji wa Miradi

Maelezo	Kiasi (Sh.Tz.)		
	Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto	OR-TAMISEMI	SM
Salio anzia 1 Julai 2016	149,913,966	4,545,282,036.06	20,593,701,658
Ongeza: Fedha iliyopokelewa	8,768,477,000	30,085,677,840	105,827,586,360
<b>Fedha iliyokuwepo</b>	<b>8,918,390,966</b>	<b>34,630,959,876.06</b>	<b>126,970,149,017.83</b>
Matumizi yaliyofanyika	7,357,570,608	6,192,407,085.06	115,546,902,047.11
Marejesho kwenye akaunti kuu	149,913,966	-	-
Salio ishia 30 Juni 2017	1,410,906,392	28,438,552,791.00	11,423,246,969.72

Chanzo: Taarifa ya fedha inayoishia 30 Juni 2017 ya Mfuko wa Afya

### 4.3 Mfuko wa Barabara

#### 4.3.1 Utangulizi

Vyanzo vikuu vya mapato ya Bodi ya Mfuko wa Barabara ni pamoja na kodi itokanayo na mafuta, ushuru wa usafirishaji wa bidhaa na mali kwenda nje ya nchi, tozo ya kupakia mizigo kupita kiasi, riba, na mapato mengineyo, hasa kutoka Shirika la Kimataifa ya Maendeleo ya Uingereza. Fedha yote inayokusanywa kama mapato ya Mfuko wa Barabara inagawanywa kwa watekeleza miradi ya barabara ambao ni Mfuko wa Barabara, Wizara ya Ujenzi, Wakala wa Barabara wa Tanzania, OR-TAMISEMI na SM wakizingatia asilimia ya mgawanyo uliopitishwa na Bunge.

Angalau asilimia 90 ya fedha zote zilizowekwa kwenye Mfuko wa Barabara zinatakiwa zitumike kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa dharura wa barabara zilizoainishwa. Pia, fedha hizo zinatumika kwenye shughuli za kiutawala zinazohusiana na matengenezo na ukarabati kwa upande wa Tanzania Bara kulingana na mpango kazi wa utekelezaji ulioidhinishwa. Kiasi kilichosalia pia hutumika kwenye miradi ya maendeleo

ikiambatana na gharama za utawala kwa upande wa Tanzania Bara.

#### 4.3.2 Ufadhilli

Mfuko wa barabara ulikuwa na kiasi cha Sh.Tz. 870,518,855,605 ikiwemo na Sh.Tz. 92,806,884,046 kutoka kwa wafadhili kwa utekelezaji wa kazi zilizopangwa, angalia jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 7: Mwenendo wa Makusanyo ya mapato kwa Miaka**

Chanzo cha Mapato	Mwaka wa Fedha (Kiasi-Sh.Tz.)		
	2016/17	2015/16	2014/15
Ushuru wa Mafuta	744,100,055,085	705,091,411,698	623,175,176,771.09
Ushuru wa usafirishaji	11,588,549,889	9,491,496,859	7,904,356,679.48
Tozo ya kuzidisha mizigo	10,976,051,955	8,052,957,501	11,348,406,232
Shirika la maendeleo la Uingereza (DFID)	92,806,884,046	26,114,158,400	19,772,448,112
Mfuko wa hifadhi ya barabara	10,000,578,282	-	588,939,182
Mapato Mengineyo	284,678,382	278,491,547	198,310,481
Mapato yanayotokana na Riba	762,057,966	818,778,313	
<b>Jumla</b>	<b>870,518,855,605</b>	<b>749,847,294,318</b>	<b>662,987,637,457.57</b>

*Chanzo: Taarifa ya fedha ya Mfuko wa barabara inayoishia 30 Juni 2017*

Mchanganuo wa hapo juu unaonesha kuwa mwenendo wa fedha zinazopokelewa kutoka bodi ya mfuko wa barabara zimeongezeka kwa asilimia 16; na ongezeko kubwa limetokana na Shirika la Maendeleo la Uingereza na Mfuko wa Hifadhi ya Barabara kwa asilimia 255 na 100 mtawalia.

#### 4.3.3 Ufadhilli wa Mfuko wa Barabara kwa SM

SM zilikuwa na salio anzia la Sh.Tz. 54,555,130,277.46 zilipokea Sh.Tz. 219,391,809,477.54 ambapo Sh.Tz. 191,941,807,039.36 zilitumika na kubaki na salio ishia la Sh.Tz. 82,005,132,715.64 ambalo ni sawa na asilimia 30 ya fedha zilizokuwepo kwa ajili ya kukamilisha miradi iliyopangwa.

## **4.4 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya Tatu - Mpango Uhaulishaji wa Fedha kwa Kaya Maskini**

### **4.4.1 Utangulizi**

Mradi wa Maendeleo ya Jamii awamu ya tatu uliombatana na mpango wa uhaulishaji kwa kaya maskini ulianzishwa tarehe 15 June 2012 kufuatia makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo (IDA). Mfuko wa Maendeleo ya Jamii uliruhusiwa kupata mkopo wa thamani sawa na haki ya kutoa fedha (SDR) 141,900,000 inayolingana na DK 220,000,000 kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia tarehe 13 Agosti 2012 hadi tarehe 31 Desemba 2017

Mradi wa Maendeleo ya Jamii ni sehemu ya mpango mkakati wa kitaifa wa kuondoa umasikini ulioanzishwa ili kujenga uwezo wa jamii kupata fursa zinazochangia kuboresha maisha kuendana na malengo ya milenia yenyе mkakati wa kupunguza umaskini. Lengo la mradi ni kutengeneza mtandao salama wa uzalishaji wa kina, wenye ufanisi na unaolenga kaya maskini kwa jamii ya Tanzania.

### **4.4.2 Ufadhilli**

Katika Mwaka wa fedha 2016/2017 Mradi wa Maendeleo ya Jamii ulipokea jumla ya Sh.Tz. 318,577,767,464.44 Pia ulikuwa na salio anzia la Sh.Tz. 36,027,176,101.46 na kufanya jumla ya kiasi kilichokuwepo kwa matumizi kuwa Sh.Tz. 354,604,943,565.90. Aidha mradi umetumia jumla ya Sh.Tz. 324,188,446,473.51 (inajumuisha fedha zilizopelekwa kwa watekeleza miradi) hivyo kubakiwa na kiasi cha Sh.Tz. 30,416,497,092.39, maelezo zaidi yanaoneshwa kwenye jedwali hapo chini:

**Jedwali Na. 8: Ufadhili wa Mfuko Mradi wa Maendeleo ya Jamii**

